# Gazeti la Kimataifa

## Waabuduo Damu ya Kristo

…Kwa Neno Lako…
Lima, Peru
5–28 Luglio 2017

Mwaka XXI – N. 9, Oktoba 2019

ASC Mawasiliano ya Kimataifa – Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias, 10 - 00183 Roma

www.adoratrici-asc.org
redazioneasc@adoratrici-asc.org

Mhariri

# Kusubiri ni sawa na uvumilivu



Neno la Kihispania "esperar" linamaanisha kungojea kwa sababu, kungojea pia ni kutumaini. Kwa hivyo, kujua jinsi ya kungoja inahitaji nguvu kubwa ya roho, ambayo inamaanisha kipimo kizuri cha uvumilivu, uwezo wa kuendelea kusimama ili kupokea mazingira ya ulimwengu kwa njia iliyo ya haki zaidi.

Watu wanaweza kujikuta tena wavumilivu, wanaweza kusikiliza na kusikilizwa, wanaweza kugundua hofu zao bila hizo hofu kuwashinda, na matarajio yao bila kudanganywa, kwa sababu kungoja ni chombo bora cha kuingia kwenye sala. Lakini, siyo hali ya kutokuwa na nguvu kabisa. Ni kama mkulima anayepanda na hutunza bustani yake kila wakati na kwa bidii. Anafanya kazi bila kukoma, lakini ni dhahiri kwamba katika kazi yake anasubiri kwa uvumilivu na matumaini, lakini zaidi ya yote, husali. Ni dhahiri katika uwezo wa kuheshimu majira ya Mama Mazingira asili ambako ladha nzuri ya zawadi tunazopewa imefichika. Hata ingawa mwili wake unajibu kwa uchovu wa kila siku, moyo wake una amani na anaweza kutambua kweli ishara za Mungu Mpaji.

Siku hizi, hata hivyo, sisi, watoto wa jamii ya kisasa, tunakimbia kwa hasira, kila wakati tunakimbia kila mahali kana kwamba hakuna muda wa kutosha na kwa hivyo hatusimami kamwe. Kukimbia huku na huko hakutuweki katika nafasi ya kutafakari, tunashindwa kujithibiti kwa urahisi sisi wenyewe, kwa hiyo tunakuwa dhaifu zaidi; pia tunaugua, tena kwa haraka. Tunakuwa na vita ndani ya nafsi zetu wenyewe na wengine, na viumbe. Hatuwajali tena jirani zetu kwa sababu ya haraka zetu za hapa na pale zinazotupelekea kushawishika kwamba hatumhitaji jirani yetu. Kupoteza uvumilivu imekuwa janga la kijamii, kwa sababu hakutupeleki tu mbali na Mungu, bali pia hutuondolea hali ya kutambua maana na umuhimu wa binadamu.

Kwa hiyo, wakati huu ambapo mabadiliko kati ya majira yanawakilisha kungoja nyakati mpya, Yesu anatualika kugundua tena utulivu wa roho, kuingia kwenye ukimya wa kina. Anatualika tukae karibu naye ili tuweze kuelewa ni kiasi gani neno na Neno ni muhimu sana katika kufikia dhamiri za wengine. Kristo anatuhimiza tutulize wasiwasi wetu wa ndani ili kupata tena amani inayofaa inayoweza kutupeleka kwenye sala, kwenye wokovu. Anashauri utambuzi kama njia pekee ya kujiboresha sisi wenyewe kama wanadamu na wakristo. Anatufundisha kupumua kwa utulivu, bila woga wowote. Anatufundisha kuwa Upendo huzaliwa ndani ya mioyo minyofu na minyenyekevu, ya wale ambao wamejifunza kungoja, kuwa na uvumilivu. Anatufundisha kwamba sala na mazungumzo yanayohitajika na Baba hutupatia kipimo sahihi cha sisi ni nani: binti wapendwa wa Mungu. Kwa msalaba wake, Yesu Kristo ametuonesha kuwa tumaini halifi kamwe kwa wale wanaojua "kuvumilia."

***Sr. Maria Grazia Boccamazzo, ASC***

## Muhstasari

*Mhariri*
◇ Kusubiri ni sawa na uvumilivu 1
*Nafasi kwa Uongozi Mkuu*
◇ Novisiati ya Shirika – Jumuiya ya Malezi 2
*Toka Ulimwengu ASC*
◇ "Alishafika huko kabla yetu" 3
◇ Tuzo ya Heshima 3
◇ Matembezi ya Septemba 4
◇ Dayton imara 5
◇ Mang'amuzi ya pekee kwenye Ashram 6
◇ Mang'amuzi kutoka Kituo cha Don Bosco 7
◇ Miaka 20 ya Uwepo wa ASC Belarus 8
*Nafasi kwa JPIC/VIVAT*
◇ "Amazon: Njia Mpya kwa Kanisa na kwa Maunganiko wa Ekolojia" 9
◇ Mbali na uchakataji tena … Namna ya kulinda Mazingira yetu 10
*Ndani ya Shirika*
◇ Siku za kuzaliwa: Tunasherehekea Maisha 11
◇ Waliorudi Nyumbani kwa Baba 11

## Novisiati ya Shirika – Jumuiya ya Malezi



Kwa furaha kubwa na shukrani nyingi, tulishiriki katika kuhamia kwa Masista wetu kwenye jumuiya ya novisiati wakati wa siku za kwanza za Septemba: Sr. Mariamma Kunnackal, ASC, Sr. Emanuela Škarica, ASC, Sr. Joan Stoverink, ASC, Sr. Marisa Nardoni , ASC na Sr. Martha Josefu Kwimba, ASC.

Walihama kutoka Nyumba Kuu na kwenda kwenye Nyumba ya Novisiati ya Shirika, via Giuseppe Gatti n.13, Sant'Agnese - Roma, ili kuanza matayarisho yote ya ujio wa wapostulanti wa kwanza, watakaokuja kwa alili ya uzoefu wa kwanza wa mwingiliano wa tamaduni wa malezi katika Shirika. Ilipendeza sana kuwaona wakiwa na ari na umakini katika kujiandaa kukumbatia mang'amuzi mapya. Kila mmoja anajenga mahusiano kwa umakini ili kuondoa tofauti za kitamaduni na utamaduni wa ASC.

Kwa shauku kubwa na ushiriki, wanajumuiya wote wa Jumuiya ya Kimataifa walishiriki katika wakati huu wa mwanzo wa safari muhimu ya malezi ya Shitika ya mwingiliano wa kitamaduni. Kila mmoja aling'amua kwa kina utekelezaji wa hamu yetu sote tuliyoielezea kwenye Hati ya Mkutano Mkuu wa 2017: Novisiati moja ya Shirika.

Kwa namna ya pekee, sisi, kama Uongozi Mkuu, pia tuling'amua nyakati hizi kwa shukrani kwa Bwana na kwa matumaini kwamba mchakato huu unaweza kuhusisha Shirika zima.

Kwenye Hati, tulionyesha hamu ya kusonga mbele kama mwili mmoja na hii inatusaidia kuamini kuwa tunaweza kuwa ishara kwa ulimwengu huu, kwa kujenga vizazi vipya vya ASC ili waweze kuwa Mitume-Waabuduo wenye upendo na hodari.

Tunamshukuru kila mmoja wenu kwa ushiriki wenu hai ambao unatufanya tujisikie kuungwa mkono na kusindikizwa. Tunaukabidhi mwanzo wa Jumuiya ya Novisiati ya Shirika katika sala zenu.

***Sr. Matija Pavić, ASC***



Eneo la Bara: Afrika
Region ya Tanzania

## "Alishafika huko kabla yetu"



Katika maandalizi ya kusherehekea miaka 50 ya uwepo wa MasistaWaabuduo Damu ya Kristo, Tanzania, tulipanga kutembelea sehemu mbalimbali na makundi ya watu, kwa namna ya pekee yale yenye majina na yanayosimamiwa na Mt. Maria De Mattias.

Lengo letu lilikuwa ni kushirikishana nao Karama na Roho ya Shirika letu, kuwasaidia ili waweze kumfahamu Mt. Maria De Mattias, na kwa namna ya pekee "kumfahamu Yesu na kumpenda, kulingana na ndoto ya Mt. Maria De Mattias.

Tayari tulishatembelea na kuinjilisha makundi 11 na jumuiya ndogondogo za Kikristo, vigango vitatu, parokia moja na kwaya 5 zenye jina la Mt. Maria De Mattias. Licha ya makundi haya tuliinjilisha sehemu zingine mahali tulipo.

Katika mchakato wa mpango huu, tuligundua kuwa, katika maeneo kadhaa, watu walimchagua Mt. Maria De Mattias kuwa msimamizi wao, lakini hawamfahamu vizuri. Moja ya sehemu hizi ni kigango cha Kitalalo ambacho kipo kwenye Parokia ya Kintinku ambayo kwa sasa inhudumiwana Mapadri wa Jimbo la Singida. Baada ya kupewa taarifa na Masista wa Misericordia ambao walikuwa wanakifahamu Kigango hiki, tulipanga kukitembelea.

Ilikuwa Jumapili, mwezi Agosti, 18, 2019, Sr. Theresia Rogatus, Sr. Martina Marco na Sr. Margareth Silvery walienda huko mapema asubuhi na waliweza kusali pamoja na waamini wakigango hiki. Tulikaribishwa vizuri. Walifurahi sana kuweza kumfahamu Mt. Maria De Mattias, Karama na Roho ya Shirika. Walitusimulia historia ya Kigango chao chenye jina la Mt. Maria De Mattias. Walisema, walimfahamu Mt. Maria De Mattias kupitia Wamisionari wa Damu Azizi, kwa sababu wakati huo parokia yao ilikuwa ikihudumiwa na Mapadri wa Damu Azizi na wakati huo paroko wao alikuwa Padre Chrisogon, CPPS. Ni yeye ambaye alimtambulisha Mt. Maria De Mattias kwao wakatia lipotangazwa Mtakatifu mwaka 2003, na kuwashauri kumchagua kama msimamizi wao. Hivyo toka wakati huo wanamheshimu mtakatifu huyu kama msimamizi na mwombezi wao.

Tulishangaa sana, kwa sababu hili ni eneo lililoko mbali na halina hudumu kadhaa za kijamii kwa ujumla ni eneo maskini, lakini Mt. Maria De Mattias tayaria likuwa pale pamoja na watu hawa. Huyu mwanamke shujaa anatupa changamoto kwamba, tunapaswa kujitahidi siku hata siku kuwafikia watu wale ambao hawana mtu wa kuwasaidia ili kuwasaidia kumjua na kumpenda Mpenzi wetu Yesu.

***Sr. Margareth S. Ngoi, ASC***

Eneo la Bara: Amerika
Region ya Manaus

## Tuzo ya Heshima

Mwaka huu Masista ASC wawili wa Region ya Brazil walitunukiwa tuzo ijulikanayo kama HONOR WHERE HONOR IS DUE kwa huduma yao katika nyanja ya elimu.

Mnamo Mei 23, 2019, Chuo cha Amazoni cha Fasihi kilitaka kutoa heshima kwa kikundi cha watu waliochaguliwa kutoka kwenye duru ya tamaduni na siasa wa mji wa Manaus kwenye maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka 100 ya kuanzishwa kwake. Wakati wa hafla nzuri, walitunukiwa medali ya karne moja. Sista Marilia Menezes alikuwa mmoja wa hao watu waliotunukiwa heshima hiyo. Kwa kuwa hakuweza kusafiri kwenda kwenye hafla hiyo kwa sababu anaishi Belém, alimwomba Sr. Clara kupokea medali hiyo kwa niaba yake. Sherehe hiyo ilikuwa ya kukumbukwa kweli!

Mnamo Agosti 30 wakati wa mkutano rasmi, Halmashauri ya Jiji la Manaus, kupitia ombi la diwani wa jiji, iliruhusu mtu mwingine kuchukua medali ya dhahabu kwa niaba ya Sista wetu Maria da Paz Azevedo aliyotolewa na patron Gracitylzo do Lago Silva. Sherehe hiyo ilifanyika wakati wa kikao cha mkutano katika Ukumbi wa Jiji la Manaus.

Katika shukrani zake, Sr. Maria da Paz alimnukuu mtoa elimu mkuu, Paulo Freire, "Si katika ukimya kwamba watu wanaundwa, bali kwa maneno, kazi na hatua za tafakari." Ni kile alichosema Mt. John Bosco, "elimu ni jambo la moyo."

Kila la heri kwa Masista hawa na ASC wote ambao walitolea maisha yao yote kwa ajili ya huduma kwa wengine, hasa katika nyanja ya elimu, wakifuata hatua za Mt. Maria De Mattias.

***Sr. Clara de Albuquerque Silva, ASC***



# Matembezi ya Septemba

*Ujumbe wa Mhariri: Hayati Janis Yaekel, mpenzi wa mazingira ya asili na ndege, alikuwa akipenda kutazama ndege wadogo nje ya chumba chake huko Clementine Hall kwenye Nyumba ya Ruma. Baada ya kufariki mwaka jana, wafanyakazi waliandaa nafasi kwa ajili ya kutazama ndege kutoka chumba cha kulala kisichokuwa na shughuli. Viti vya chumba cha kulala na vitabu vya ndege wadogo vilichukua nafasi ya samani za chumba cha kulala. Dada yake Sr. Georgia Kampwerth, ASC, amekuwa mwangalifu kuhakikisha kuna malisho ya kutosha. Yeye husaidiwa na Paula Hall, mfanyikazi hodari.*

Ukiangalia mmoja kwenye kalenda ya Septemba inaonyesha usawa kati ya Mchana na Usiku (Equinox) mwezi Septemba na dalili dhahiri za kumalizika kwa majira ya joto na kuanza kwa vuli. Kama Mississippi ya zamani, tunaendelea tu kuzunguka! Lakini ni wakati mzuri wa kurudisha nguvu zetu katika Msimu huu mzuri wa Uumbaji ulioanza Septemba 1 na unaendelea hadi Oktoba 4, Sikukuu ya Mtakatifu Francisco wa Assisi.

Mtakatifu Francisco anatukumbusha kwamba kuna vitabu viwili vya kutusaidia kumjua Mungu: Kitabu cha Maandiko Matakatifu na Kitabu cha Mazingira ya Asili. Papa Francis katika Barua yake, Laudato Si', anatukumbusha kwamba uumbaji wote ni mahali pa kukutana na Mungu, akibainisha kuwa "Francisco wa Assisi anatupeleka kwenye moyo wa kujua kuwa wanadamu. Aliongea na viumbe vyote, akiwaita ndugu na kuwaheshimu wote kwa adabu na heshima."

Ziara ya hivi karibuni kwenye chumba cha kutazama ndege wadogo wazuri, ilionekana kuwa bado kuna maisha na shughuli nyingi zinaendelea katika uumbaji huko Ruma. Ilikuwa ni mara ya kwanza mimi kusimama na kutazama shughuli za "mafundi" na kuhisi kana kwamba nilikuwa kwenye kanisa kuu. Ilikuwa takatifu, ya kushangaza na ya kuvutia. Iliamsha sala ya Papa Francis kwa ajili ya Dunia yetu: "Ee Mungu wewe upo katika ulimwengu wote na katika viumbe vyako vilivyo vidogo sana."

Ndiyo, viumbe hivi vidogo vinahitaji ulinzi wetu na utunzaji. Asante, Sista Georgia Kampwerth na Paula Hall! Ni zawadi gani mmetupatia kuchukua jukumu la kutunza hizi alama za Mungu kati yetu. Nilikaa kwa mshangao, kwa kustaajabia na kwa shukrani wakati nikiangalia uwepo wao, uzuri, na shughuli zao na kufanya "mahali patakatifu" pabadilike mara moja ndani yangu, ndani ya wengine na Mungu. Sidhani kama kuna utengano! Bali kuna muunganiko.

Hakika, ikiwa mtu anatembea ndani ya chumba cha kutazama ndege wadogo na anachukua muda wa kuwa pale, tazama, ataondoka akiwa na shukrani ya kina na furaha ambayo mazingira ya asili hutoa na atakumbatia utakatifu kwa wakati huu. Kutunza na kukuza uumbaji ni uhai.

Nilisoma mahali pengine kwamba ndege wadogo wazuri peke yao wanauwezo wa kuruka kwa mabawa yao kwa mfano wa ishara ya umilele au umbo la 8. Kwa hivyo, ni ishara ya umilele, hali isiyo na mwisho na isiyo na kikomo. Kutembea ndani ya chumba, hewa ikiwa imewashwa, malisho ni safi, na yaliyojazwa vizuri na uwepo wa ndege wadogo utatoka nje ukiwa hai zaidi na kupatana na wote, kuliko kabla ya kuingia chumbani. Kama Gerard M. Hopkins alivyoandika, "Ulimwengu unawajibika kutambua ukuu wa Mungu." Ninaongezea, na tuwe na uelewa zaidi juu ya mtandao wenye sehemu nyingi wa maisha ambao unatuunganisha sote.

***Sr. Mary Shaw, ASC***



# Dayton imara

*Kamati ya Tasaufi ya Damu, Tafakari ya Septemba*

Ni majira ya joto huko Dayton, Ohio. Yalianza Mei 25 wakati Ku Klux Klan alipofanya mkutano katika Uwanja wa Mahakama huko Dayton katikati ya jiji. Siku kadhaa baada ya Nchi ya Montgomery kutoa kibali kwa kikundi cha Ukoo kukutana kwenye Uwanja wa Courton wa Mahakama ya Dayton, mkusanyiko wa vikundi vya jumuiya uliongeza juhudi za kupinga tukio lililopangwa. Mwishowe, washiriki wa koo tisa walijitokeza kama walivyofanya, waandamanaji karibu wa 600 ambao walisema hakuna nafasi ya chuki huko Dayton. Nilijivunia mji wetu.

Halafu Siku ya Kumbukumbu, baada ya siku ya kupendeza ya pikniki na safari, hali ya hewa iligeuka kuwa mbaya usiku huo. Vimbunga kumi na tano viliharibu sehemu za jiji, hasa maeneo yenye kipato cha chini. Vyumba vingi, nyumba, na biashara ziliharibiwa. Kiasi cha uharibifu hakikujulikana kabisa hadi asubuhi iliyofuata. Miti mingi ilianguka chini, nyumba zilibaki bila paa na sehemu za majengo zilikuwa barabarani na kwenye bustani nzuri za majani. Kituo cha kusukuma maji kiliharibiwa, na kusababisha kukatika kwa maji na umeme kwa siku. Watu wa Dayton walipita na walitoa maji, chakula na pesa. Watu wanaojitolea walipiga hema karibu na maeneo yaliyoharibika zaidi ili kutoa maji na chakula kwa watu wengine wanaojitolea kufanya kazi ya kusafisha uchafu wa kimbunga. Tena, nilijivunia mji wetu.

Mnamo Agosti 4, tuliamkia kwenye habari mbaya kwamba watu tisa wameuawa kwa kupigwa risasi katika uwanja wa burudani wa mji wa Wilaya ya Oregon, ndani ya masaa 24 baada ya watu 22 kuuawa katika shambulio lingine la watu huko El Paso, Texas. Mpiga risasi aliuawa na Polisi wa Dayton, na kuongeza idadi ya vifo kuwa watu 10. Tena, mji uliungana kwa ajili ya mkesha usiku huo katika Wilaya ya Oregon kusali kwa ajili ya wahanga na kwa ajili ya mji. Njia ilikuwa zimejaa watu, waliokusanyika kuomboleza na kujaribu kuelewa kuwa jambo hili limeweza kutokea hapa. Tena, nilijivunia mji wetu, Nguvu ya Dayton.

Kama Shirika, hatungeweza kukaa kimya mbele ya janga baya kama hilo. Halmashauri yetu mpya ya Jumuiya iliyochaguliwa ilitoa taarifa kwa waandishi wa habari ambayo inasema kwamba "tunaimarisha azimio letu la kukabiliana na kushinda vishawishi vibaya katika utamaduni wetu ambao husababisha vurugu hizi na kudai sheria nzuri zinazofanya kazi kwa faida ya watu wote, siyo kwa wachache wenye nguvu. Tunaamini kuwa kila mtu ni wa thamani machoni pa Mungu, hata wale wanaofanya vitendo vya dhuluma. Kama Daytonia, El Pasoans na wengine wengi ambao wamekuwa wakionyesha, tuendelee kuonesha kuwatunza na kuwajali majirani zetu, hasa wale walioko pembezoni mwa jamii. Kwa kufanya hivi, kwa pamoja tunaunda jamii yenye amani zaidi na yenye upendo ambapo nguvu ya upendo, siyo chuki, ni ushindi. "

Inaonekana kwamba kila siku hutokea janga mpya, kumwaga damu bila sababu kwa vurugu. Kama watu waliowekwa wakfu kwa Damu ya Thamani ya Yesu, tumeitwa, wakati huu katika nchi yetu na katika ulimwengu wetu, kuwa mashahidi wa upendo wa Mungu unapatanisha na kukomboa, ambapo labda katika safari huko nyuma hatujawahi kufanya hivyo. Ni changamoto kubwa kwetu. Tuzipokee changamoto!

***Sr. Ann Clark, CPPS, Dayton***



Eneo la Bara: Asia
Region ya India

# Mang'amuzi ya pekee kwenye Ashram

Tunaona mwanga wa siku na njia ya mageuzi, ubunifu, utambuzi wa kina, ya kusikiliza na ya maongozi ya Mungu. Kuomba huruma na kutafuta neema, ambayo siyo tu ya wakati wa kufaa bali pia inaambatana na mafundisho ya Papa Francis na kwa kweli haya yalikuwa nimang'amuzi yaliyosawa na yetu pia.

Sisi wanovisi, pamoja na mlezi wetu Sr. Marykutty Kanattu tulikwenda Anjali Ashram-Mysuru, ambayo iko karibu na kilima cha Chamundi. Kwa kweli tulipata mang'amuzi ya pekee na yenye utajiri. Tulikuwa na siku kumi, lakini hatukuweza kutambua jinsi siku zilivyopita haraka. Washiriki wa mpango huo walikuwa 32. Washiriki wote walikuwa na heshima kwa Atma- Poorna -Anubhava (Utambuzi wa jumla wa Nafsi). Mpango huu ulianza na adhimisho la Misa Takatifu ya Kihindi, kwa ishara zote za kukaribisha, utakaso na uwashaji wa taa ya India.

**Njia ya maisha ya Ashram** inaalika kuishi fumbo la Pasaka, ambapo watu wanaitwa kuwa na shauku ya Mungu. Tunaiishi kwa kwa kuunganisha **Dhyana (Tafakari), Upadhesa (mafundisho) na Seva (Huduma).** Waliishi **Jnanamarga, Bhakti Marga na Karma Marga (Sehemu ya Uchaji, sehemu ya Kujitolea na Sehemu ya Huduma).** Ukweli, ukimya na ufahamu yalikuwa ni maneno makuu, kuishi changamoto zake na masharti yake. Siku ya kwanza kabisa tuliongozwa vyema na Fr. Louis, kutunza ukimya na upweke. Tulipoanza safari yetu ya mang'amuzi ya Ashram, tulielekeza mwelekeo wetu juu ya - kuwa na mang'amuzi ya juukabisa. Mwongozo wetu mzuri ulituweka kwenye mahali sahihi. **"Mioyo yetu haitatulia mpaka imetulia ndani yako"**. Maisha ya mifano ya Watakatifu yaliundwa ndani yetu hamu ya kukutana na Bwana moyoni mwetu. Kila siku, tulikuwa na mafundisho tofauti, kusoma, kutafakari, mashairi, na maandiko ya dini tofauti kwa kutafakari yetu.

Ukimya na utulivu ulituwezesha kugundua uwepo wa Mungu, ulitoa ujuzi na ufahamu juu nafsi. Mafundisho juu ya uhuru yalitusaidia kugundua kuwa, sisi ni watoto wa Mungu na mazungumzo juu ya maisha ya kujitolea, yalitupa changamoto ya kujitayarisha kwa utume wake na kutusaidiakuelewa zaidi juu ya maisha ya kitawa, ambayo yalitupa mwanga zaidi kujitambua wenyewe na kutufanya tuwe watu wa hali ya juu kuhusu ukweli wa ulimwengu kwa jumla.

'Hakuna maana ya maisha, isipokuwa maana unayoyapa maisha yako, kwa kufunua nguvu isiyo na mipaka'. Usemi huu ulituangazia kuthamini uwezo wetu wenyewe na uwezo. Siku ya mwisho, tulifundishwa kwamba mwanafunzi anapaswa kuwa - wa mwisho, wa wote, huru, mkamilifu, bila masharti, imara, na mwenye thamani (mwenye malengo, thabiti nguvu na mwenye mvuto.) Madhyan Sandhya (tafakari ya mchana wa mchana tuliyoifanya chini ya mtini, mti wa walnut, na kwenye hekalu la heri pamoja na Mwalimu wetu kwa kweli ilitupatia mang'amuzi ya pekee na ya moyo na kutuunganisha na mazingira ya asili, Mungu na mkutano wetu. Mawazo ya kukaa kando ya maua ya yungiyungi ya kanisa yalitufanya tukutane na Bwana katika kina cha mioyo yetu.

Siku ya mwisho tulikuwa na ibada ya toba na ibada ya sala ya ishara ya hitimisho. Huduma ya sala ilituimarisha ili tukumbuke wema wa Mungu wa kipindi cha siku kumi zilizopita na tumshukuru kwa usindikizaji wake katika shughuli zetu zote na kwa mang'amuzi yenye utajiri ya ushirika na ushiriki.

**Mafunzo yetu ni:**

- **'Atmapur na Anubhava'** maana yake kujitambua mwenyewe. Kama watu binafsi kwanza, ni lazima kugundua nafsi yetu ya kweli na kukuza hamu na shauku kuunganika wenyewe na yule aliye mkuu kabisa – Mungu. Ni lazima tugundue nafsi yetu katika nafsi kuu kupitia ufahamu. Ubora wa ufahamu ni kipimo cha maendeleo ya kiroho ya mtu, tutakapoweza kujitambua wenyewe, tutakuwa kama Mungu wetu. Ufahamu na dhamiri ya Bwana lazima iwe kama maji ya mto yanayotiririka.
- **Lengo letu kuu katika maisha ni kumtambua Mungu.** Nafsi ya mtu ni utu na utakatifu; mtu anapoitambua na kuithamini anakuwa mtu mzuri.
- **Kuwa ni muhimu zaidi kuliko kutenda.**
- **Tulijifunza kuwa hakuna maana ya maisha isipokuwa maana tunayoyapa maisha kwa kuelezea nguvu isiyo na mwisho ndani mwetu.**
- **Kuna cheche ya ukweli katika kila dini na tunapaswa kuheshimu kila dini.**
- **Mang'amuzi ya Ashram hii kweli ya litusaidia kuchukua uamuzi wa kupenda ukimya, kuishi katika kumtambua Mungu na kuishi maisha ya kawaida; kung'amua uwepo wa Mungu katika mzingira ya asili.** Tunapenda kufanya mazoezi ya tafakari, yoga, na mazoezi ya kukaa vizuri kwa ajili ya kuwa na umakini. Tunapenda maadhimisho ya liturjia ya kihindi.

Tunapothamini kumbukumbu nzuri ya Ashram, tunamshukuru Sr. Marykutty mlezi na Masista wa Jumuiya yetu ya Novisiati na waliotusaidia kupitia sala zao.

***Wanovisi***
***Wilma, Sushma, Jennis na Maya***

# Mang'amuzi niliyopata kutoka Kituo cha Don Bosco Bangalore India

Mwezi wa nane ulikuwa ni mwezi wa pekee kwangu na wa furaha kwa ajili ya mang'amuzi niliyopata, ulikuwa ni kipindi cha Baraka kama Mt. Paulo anavyosema "namshukuru Mungu wangu kila wakati ninapowakumbuka na kuwaombea daima kwa furaha kipindi chote cha kozi katika kituo hiki cha Malezi cha Yohane.

Tulikuwa washiriki 32, kutoka Mashirika mbalimbali. Kundi kubwa la Masista walitoka katika Shirika la Mt. Anne wa Bangalore, na kundi lingune kubwa la Masista walitoka Shirika la Masista wa Upendo wa Maria Bambina, Sista mmoja toka Shirika la Ursuline, Padre mmoja na bruda kuoka Shirika la Mapadri wa Marist, Masista wawili toka Shirika la Wasalesian na mimi.



Baada ya miaka 25 nilipata nafasi hii ya kushiriki katika kozi hii pamoja kundi hili toka Mashirika mbalimba .Wengi wa washiriki wa kozi hii ni wajublei ya miaka 25 ya maisha ya wakfu. Kwa kweli ilikuwa ni kozi ya majiundo mapya kwa washiriki wote, zaidi sana kwangu mimi.

Mada mbalimbali zilizotolewa zilikuwa za kuvutia na msaada wa pekee kwangu, kama maandalizi yangu ya kupokea au kuanza utume mpya katika novisiati ya Shirika. Mada zilizofundishwa ni; uongozi wa kiroho, mbinu za kupambana na hisia za kimwili (psycho-sexual integration), maisha ya kitawa na karama ya Shirika, mageuzi ya ndani n.k.

Mada zingine zilikuwa pia msaada kwangu na nilizihitaji sana mimi binafsi kwa majiundo mapya na kwa kuihuisha roho na nafsi yangu.

Watoa mada hizo walikuwa ni wasalesian waliojiandaa vema, waliobobea na wenye maarifa tele. Walichotugawia kweli ni utajiri, Maisha halisi ya kueleweka wazi na ni msaada mkubwa kwa maisha yetu ya wakfu ya wakati wetu, tukiyatazama kwa pamoja yanatupa nguvu ya mang'amuzi yetu hasi au chanya, hisia zetu ambazo hatuzihisi tena na matatizo ambayo hatujayatatua. Imetusaidia sisi kuwa na mtazamo chanya zaidi, kujiamini, kujipokea na kukuza ujasiri wa nafsi.

Katika vipindi tofauti tofauti tulishirikishana kwenye vikundi vidogo pia vya watu wawili wawili hii ilisaidia sana pia kufahamiana kati yetu, kusaidiana na kupeana moyo.

Ninapokumbuka yote haya yaliyotendeka mwezi uliopita, ninamtukuza na kumsifu Mungu kwa Baraka zake zisizo na idadi. Ameniongoza katika njia yangu amekuwa mwanga na kiongozi, Amenitajirisha katika hatua mbalimbali, Amenipa ujasiri hasa kwa sasa ninapoelekea kuchukua wajibu katika novisiati ya Shirika.

Nachukua nafasi hii kumshukuru Sr. Nadia Coppa Mkuu wa shirika na Washauri kwenye Uongozi Mkuu kwa kunipa nafasi hii. Asanteni sana. Pia natoa shukrani kwa Sr. Mini Pallippadan, Mkuu wa Region na Washauri wake kwa kunisaidia kuchagua kozi hii na kwa ushirikiano wenu, kunitia moyo na upendo wenu na kunitunza. Asanteni sana.

Shukrani nyingi kwa ASC wote kwa sala zenu za daima zinazotubeba katika kuanzisha Novisiati mpya ya Shirika ambayo itaanza hivi karibuni.

Kwa furaha na moyo wa shukrani,

***Sr. Mariamma Kunnackal, ASC***

*Eneo la Bara: Ulaya*
*Region ya Wroctaw*

# Miaka 20 ya Uwepo wa Waabuduo Damu ya Kristo (ASC) Belarus



Tarehe 26, Agosti mwaka 1999, Masista ASC wawili kutoka Poland Sr. Ewa Piworiska na Sr.Matgorzata Augustyn walivuka mipaka ya nchi yao na kwenda kuanza utume huko Dokszyce, Belarus. Walifika huko kwa shukrani kwa mwaliko wa padre Jan F. Shirika la Mapadri wa Friars Minor Capuchins na waliishi katika chumba kidogo cha mapadre Wakapuchini ambacho kilijengwa karibu na Kanisa. ASC hao walifanya utume mbalimbali, kufundisha katekisimu, sala za kila siku kwa watoto na vijana, kuandaa watu wazima kwa sakramenti na kufanya kazi sakristia.

Mwaka 2001 walianza kujenga nyumba ya ghorofa si kwa ajili yao tu bali pia kama kituo cha kazi mbalimbali za kitume.

Tarehe 14, Septemba 2003, nyumba ilifunguliwa rasmi na Askofu Wladyslaw wa jimbo la Vitebsk. Toka wakati huo nyumba yetu imetumika kufanyia mikutano, makongamano na siku za sala kwa watoto na vijana badaye tulifungua mpango wa masomo ya ziada baada ya shule.

Kwa sasa masista watatu wanafanya utume Dokszyce ambao wa kwanza Sr. Malgorzata Augustyn toka Polandi na wawili toka Belarus, Sr. Hanna Dziatlik na Sr. Nadzieja Raczyckaja.

Tarehe 25 mwezi wa 8 tulikuwa na sherehe ya shukrani kwa miaka 20 uwepo wa ASC hapa Belarus. Muda wa pekee sana ulikuwa ni adhimisho la Misa Takatifu ikiongozwa na Askofu Alieg Butkiewick, kutoka jimbo la Vitebsk aliyeadhimisha mafumbo matakatifu. Katika mahubiri yake alisisitiza thamani ya ibada kwa Damu ya Kristo ambayo ina nguvu kubwa ya kuleta mageuzi, kutakasa, kusafisha na kuokoa.

Ilikuwa furaha kubwa kwetu kwa madhimisho hayo na kwa uwepo wa Sr. Bridget Pulickakunnel ASC, Mshauri Mkuu, Sr. Ewa Kleps ASC Mkuu wa Region na Sr. Bozena Matomisz ASC, Katibu wa Region.

Mshauri Mkuu wa Kapuchini kutoka Roma, Mlezi wa The Belarus Guardian na Mapadri wa jumuiya za karibu hapa Belarus pia walishiriki katika adhimisho la Misa Takatifu.

Misa takatifu ilipambwa kwa nyimbo zilizoimbwa na kwaya za watoto na watu wazima. Kabla ya Baraka Sr. Bridget aliwashukuru wanaparokia pamoja na wakapuchini kwa ushirikiano na misaada yao. Katika kuwaasa alisisitiza juu ya wito, hasa wale wanaotaka kujiunga alisema "kuna watu ambao Mungu anawaita kwa huduma za pekee wapo kati yetu, aliwaalika wote kuombea miito pia aliziomba familia zisiogope kuwatoa mabinti zao kwa ajili ya Mungu.

Mshauri Mkuu wa Kapuchini ambaye alikuwa Mkuu wa Province wakati tulipoanza utume wetu kwa ushirikiano pia alitoa neno la shukrani. Aliwashukuru masista kwa kazi zao za majitoleo, alikumbusha mwanzo masista walivyofika kwa furaha Dokszyce, hawakutafuta raha bali walitaka kumtumikia Mungu na wapendwa jirani zao.

Baada ya Misa ilisomwa historia ya Mt. Maria de Mattias, ilielezea wito wake, kazi alizofanya na miujiza iliyofanyika katika maisha yake. Walimwonesha Mt. Maria de Mattias kuwa nabii wa wakati wake, mwanamke wa neno. Maonesho hayo yalisindikizwa na michezo iliyooneshwa na watoto na vijana wa parokia.

Maneno ya Upendo yaliyojaa Shukrani pamoja na maua kutoka kwa wanaparokia na watoto, ilikuwa mshangao na furaha ya pekee kwetu masista. Pia walionesha na kueleza utume wetu hapa Belarus na kutupatia keki kubwa yakuvutia.

Siku hii ilijaa furaha na shukrani kwa zawadi na neema nyingi alizotujalia Mungu kwa miaka hii 20 .

Kwa uwepo wa Sr. Bridget ambaye alitoka Roma na Masista waliofika toka Poland tulijisikia tumeungana na Shirika zima.

Pia tunataka kumshukuru Sr. Nadia Coppa ASC Mkuu wa Shirika letu kwa kutukumbuka na kwa sala zake kwetu, katika sherehe hii ametupatia sanamu nzuri sana ya Mama wa Mungu kwa ajili ya jumuiya yetu.

***Sr. Nadzieja Raczyckaja, ASC***
***Sr. Hanna Dziatlik, ASC***



# "Amazon: Njia mpya kwa Kanisa na kwa munganiko wa Ekologia"

## Oktoba 6- 27- 2019

Binadamu ni sehemu ya mfumo wa ekolojia ambao unapelekea mahusiano yanayotoa uhai kwa sayari yetu; Kwa hiyo utunzaji wa viumbe hivi ni muhimu sana. Na ni msingi katika kuinua utu wa mtu na ustawi wa jamii na kutunza mazingira. Njia ya kweli ya munganiko wa viumbe hai daima inakuwa ni ya jamii, lazima ihusianishe maswala ya haki katika mjadala wa mazingira ili kusikia kilio cha dunia na cha maskini. Hiki ndicho Papa anakiita mwingiliano wa ekologia.

Amazonia ni mkoa wenye eneo la mraba km million 7.8. Inajumuisha maeneo yanayomilikiwa na nchi tisa tofauti; Brazil, Bolivia, Peru, Ecuador, Colombia, Venezuela, Guyana, Suriname, na French Guyana. Misitu yake ya asili (km milioni 5.3 za mraba) ni chanzo kikubwa cha maji salama kuliko vyote duniani na cha pekee kabisa kwa maji safi, hewa ya oksijeni kwa viumbe hai mbalimbali vya sayari yetu.

Amazon ni eneo salama kwa afya tangu historia ya zama za kale na la mafanikio. Ingawa kutokana na mwingiliano ambao hatuwezi kuepuka, uvamizi na uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na viwanda umepelekea hali ya mabadiliko ya tabia ya nchi na pia kwa kutojali kabisa kwa mamlaka zinazohusika na afya za watu, kumesababisha magonjwa mapya yameibuka. Mpango wa maendeleo unakazia tu uchumi wa kinyonyaji wa uvunaji wa misitu, uchimbaji madini na gasi asilia kama utajiri wa Pan – Amazon unaadhiri viumbe vya Amazon, jamii zao na dunia nzima.

Kilio cha Amazon kiliita Sinodi ya Maskofu kutoa majibu mapya kwa hali mbalimbali na kutafuta mbinu mpya ambazo zitaifanya Kairos ifae kwa Kanisa na ulimwengu. Sisi Waabuduo Damu ya Kristo, tunajisikia kuwa na wajibu wa kuwasaidia watu wa Amazon na Sinodi kupitia sala zetu. Naambatanisha sala kwa lengo hili. Kila Jumuiya inaweza kutafuta muda wa kusali kwa nia hii maalumu.

### SALA KWA AJILI YA MAANDALIZI YA SINODI YA AMAZON

Bwana, lisaidie Kanisa kuwasikiliza
Watu wa Amazon,
Na kutatua pamoja nao tatizo la
uharibifu unaowakabili
watu na mazingira.

Amazon pamoja na viumbe hai mbalimbali
Na utajiri wa tamaduni
Ni "kioo cha wanadamu wote"
Ili kuilinda, lazima wote tufanye mabadiliko – ndani yetu wenyewe,
Ndani ya mataifa yetu
Na ndani ya Kanisa.

Tunapofanya safari ya
Laudato Si iliyotolewa kwetu,
Tuweze kutambua zaidi
Madhara ya ekolojia na tamaduni ya
Bonde la Amazon,
Na kujifunza namna ya kuwa watunzaji na wasimamizi bora wa viumbe.
Tuweze kusimama kwa ujasiri
Kupinga uvunjaji wa haki, pamoja na:
Kupoteza ardhi, unyonyaji, tishio kwa viumbe mbalimbali
na uingizaji wa mitindo ya tamaduni na uchumi ya kigeni isiyofaa kila mahali
kwa maisha ya wenyeji.

Tufundishe namna ya kusikiliza kwa makini,
Kutenda kwa haki,
Kupenda kwa moyo,
Na kutembea kwa unyenyekevu kwenye dunia hii.

Amina

SÍNODO PARA A AMAZÔNIA

Utangulizi wa Hati ya Kazi, Sinodi ya Amazon

**Sr. Rani Padayattil, ASC**



# Mbali na uchakataji tena …
# Namna ya kulinda mazingira yetu

Chuo cha Damu Azizi cha Bari, Shule ya Ulaya ya Lugha Mbili, kwa mwaka wa masomo wa 2018/2019 kiliwasaidia watoto wa shule ya awali, msingi na secondary wa daraja la kwanza, kutafakari, kusoma na kuingia kwa undani katika mada iliyopo sasa ya ECO SUSTAINABILITY/UENDELEZAJI WA MAZINGIRA.

Kwa kuanza, walimu na watalamu waliobobea waliwasaidia wanafunzi wetu kuielewA kwa undani na kuwa karibu na dunia yetu, kutofikiri kuwa dunia ni kama mama wa kambo bali "kama dada ambaye wote tunashiriki ewepo wake na pia kama mama mzuri ambaye anatupokea kwa mikono yake"

Ni muhimu sana kuingia kwa kina kwenye mazingira ya asili ili kupata tena kumiliki na kujishikamanisha na mujiza huu na kutambua tena heshima kwa uumbaji ambapo sisi ni viumbe pekee wa Mungu.

Ilipendeza sana kuongea na watoto kuhusu viumbe mbalimbali, kutumia maji kwa uangalifu, kuheshimu mazingira, umhimu wa kuchagua mazao ya chakula, aridhi, sayansi ya viumbe na mazingira… Kwa namna ya pekee nafasi yaliyotolewa kwa ajili ya Laudato Sî ambayo ni barua ya Papa Francis, shukrani kwa Monsignor Giancarlo Bregantini aliyeongea na wazazi na watoto.

Kati ya "malengo" tumetoa elimu ya vitendo moja kwa moja kwa kuwashirikisha kikamilifu katika mazingira ya shule, tumeeleza kwa undani mambo yahusuyo mazingira, tumeamsha hamasa kwa watoto na vijana na kuwafanya kuwa wahusika wakuu wenye ujuzi wa mazingira ya asili. Upandaji wa miti ulikuwa mwanzo mzuri wa wakati ujao kama washiriki na wajenzi wa nyumba ya pamoja.

Kwa namna ya pekee sana tulitoa elimu ya Afya, usalama wa mtu binafsi na usalama wa kibinadamu kuondoa umasikini na njaa katika ulimwengu. Maisha yanahitaji umakini tangu kutungwa mimba hadi kifo pia ni muhimu kuvielimisha vizazi vipya kuwa msaada kwa maisha yanayokua na kutunza bustani ndogo walau kwa wale watakaokuja baada yetu.

Ushuhuda uliotolewa na Greta Thunberg umepelekea kuwa na "Ijumaa kwa siku zijazo"(Fridays for future) nguvu kubwa ya uhamasishaji wa kupinga mabadiliko ya tabia ya nchi, kuandaa vipeperushi na matangazo juu ya wazo letu la uzuri wa sayari yetu. 'nafikiri Migogoro juu ya tabia ya nchi/hali ya hewa ndio mgogoro mkuu ambao binadamu hajawahi kuona, kama hatutafanya kitu sasa, tunaanguka / tunapotea" alisema Greta, kwamba wakati naendelea kukua ningependa kukumbuka siku za nyuma na kusema: Nimefanya yale yaliyokuwa katika uwezo na wakati wangu maana ilikuwa lazima kufanya kila kitu kinachowezekana.

Shule ya sekondari Daraja la Kwanza Chuo cha Damu Azizi cha Bari kilimaliza kozi hii hapo tarehe 12 Juni kwa kufanya maonyesho na maigizo ya chuo chao. Maonesho hayo yalipendeza sana na yalitoa nafasi nzuri ya kurudia pamoja na wanafunzi, wazazi na marafiki hatua muhimu ambazo wanafunzi wamezipitia kwa kipindi cha mwaka, hii ni muhimu sana kwa walinzi wa viumbe. kwa hakika tukikumbuka kuwa mwaka 2020 plastiki zitateketezwa kwa moto ulimwengu wote, wanafunzi wote tumeanza, tukisaidiwa na walimu wetu kutokomeza chupa za maji za plastiki, matumizi makubwa ya maji ya chupa, vikao na watalamu wa chakula vimewafanya wasisitize zaidi afya na chakula bora…

Mashirikisho ya kuvutia zaidi yalikuwa ni tafakari kutoka kwa Sr. Ran Padayattil ASC ambaye ni mjumbe wa CIS. Ujuzi wake juu ya mada ya haki, amani na kulinda viumbe ulipata mwitikio wa nguvu kwa waliohudhuria. Ilipendeza kushirikisha namna ambavyo Waabuduo Damu ya Kristo wengi wanavyopambana kutunza nyumba ya pamoja. 'ndiyo! Asifiwe Bwana wangu, kwa ajili ya dada mama dunia, ambaye anatutunza na kutuongoza sisi, na anazalisha matunda mbalimbali na maua ya rangi nzuri za kuvutia pia dawa za asili" ni sala ya Mt. Fransis wa Asissi katika utenzi wa viumbe na msisitizo wa kusifu ni uthibitisho kwa ulimwengu kuwa kila mmoja wetu lazima amtunza mama dunia. Sisi wenyewe ni dunia (Mwa.2:7) "mwili wetu umetengemezwa kwa chembechembe za sayari, hewa yake ndio inatuwezesha kupumua na maji yake yanatupa uhai na kutufanya wapya."( Laudate Si 2.)

***Sr. Francesca Palamà, ASC***








## Siku za kuzaliwa: Tusherehekee Maisha ya:

| | | |
|---|---|---|
| 30 | | |
| **Sr. Fátima Euriza VT Mário Gomes** | 24/10/1989 | Spagna |
| 40 | | |
| **Sr. Ljubica Radovac** | 21/10/1979 | Zagabria |
| 70 | | |
| **Sr. Vicki Bergkamp** | 20/10/1949 | USA |
| 80 | | |
| **Sr. Patrizia Tagarelli** | 05/10/1939 | Italia |
| **Sr. Bianca Lorusso** | 23/10/1939 | Italia |
| **Sr. Rosa Tolve** | 24/10/1939 | Italia |
| **Sr. Eileen Dehner** | 26/10/1939 | USA |
| 100 | | |
| **Sr. Maria Novelli** | 15/10/1939 | Italia |



## Waliorudi Nyumbani kwa Baba

| | | |
|---|---|---|
| 05/09/2019 | **Sr. Thomasine Stoecklein** | USA |
| 22/09/2019 | **Sr. Teresa Perinelli** | Italia |
| 27/09/2019 | **Sr. Benigna Schurtenberger** | Schaan |


Gazeti la Kimataifa
Waabuduo Damu ya Kristo
...Kwa Neno Lako...

**Habiri ya kila mwezi**

*na*

***Waabuduo Damu ya Kristo***
***Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu***
Via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA

**Mwaka XXI, N. 9, Oktoba 2019**

*Kamati ya wahariri*
**Maria Grazia Boccamazzo, ASC**

Tafsiri na
***Sr. Klementina Barbić*** *- Kikroeshia*
***Sr. Betty Adams*** *- Kiingereza*
***Sr. Martina Marco*** *- Kiswahili*
***Sr. Bozena Hulisz*** *- Kipolishi*
***Sr. Clara Albuquerque*** *- Kireno*
***Sr. Miriam Ortiz*** *- Kihispania*
***Sr. Johanna Rubin*** *- Kijerumani*